Jarida la
# NCHI YETU
Tanzania

Limeandaliwa na Idara ya Habari - MAELEZO | Toleo #. 20

Jarida La Mtandaoni



27 MACHI, 2020

#TUMEAMUA2020

# TAHARIRI

## TAKUKURU Wanaisaidia Nchi, Wapewe Ushirikiano

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt.John Pombe Magufuli amekabidhiwa ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, pamoja na taarifa ya utendaji kazi ya Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Ikulu ya Chamwino mkoani Dodoma, ikiwa ni matakwa ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.

Mawasilisho ya taarifa hizo yameonyesha jinsi Serikali ilivyo makini na inavyosimamia suala la uwajibikaji kuanzia kwenye Ofisi za umma, mashirika, vyombo vya ulinzi na usalama na hata kwa watu binafsi.

Kwa mujibu wa Rais Magufuli, uwajibikaji na uzalendo kwa nchi ni jukumu la kila mtanzania anayependa maendeleo ndio maana akazipongeza ofisi za CAG na TAKUKURU kwa kazi nzuri ya kuokoa fedha za umma kwa maslahi ya kuwaletea wananchi maisha bora.

Ripoti ya TAKUKURU imeonyesha kurejeshwa kwa zaidi ya shilingi bilioni 8.8 za wakulima zilizokuwa zimeliwa na vyama vya ushirika baada ya Rais Magufuli kuagiza uchunguzi wa kina ufanyike na wakulima wapate haki yao.

Mapambano dhidi ya rushwa na ufisadi sio vita ya kuwaachia TAKUKURU peke yao, ndio maana Rais Magufuli akawashangaa viongozi ambao vyama vya ushirika viko katika maeneo yao kwamba ilikuaje wasubiri TAKUKURU waje wapambane kurudisha fedha walizodhulumiwa wakulima wakati wao wapo na wanalipwa mishahara.

Hima Watanzania tukemee na kuchukia rushwa kwani ni adui wa haki na maendeleo ya Taifa letu hasa katika kipindi hiki ambacho maendeleo makubwa na ya haraka yanaonekana chini ya Serikali ya Awamu ya Tano. Hongera TAKUKURU wananchi tuwaunge mkono katika mapambano haya kwani umoja ni nguvu na kwa pamoja tutashinda.



# JPM Amelitendea Haki Jiji la Dodoma

Kazi kubwa zimefanywa na Serikali ya Awamu ya Tano chini ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Magufuli kwa kujenga kisasa Mji wa Dodoma katika sekta mbalimbali ikiwemo miundombinu, afya, elimu na kufungua fursa za kiuchumi Wilaya ya Dodoma.

Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Patrobas Katambi ameelezea juu ya mipango yake ili kutimiza azma ya Rais Magufuli ya kuhakikisha Dodoma linakuwa Jiji la Kimataifa. Aidha, shilingi bilioni 52 zimetengwa kwa ajili ya masuala mbalimbali ya wilaya hiyo ambapo kwa mujibu wa Katambi kiasi cha shilingi bilioni 17.3 zimetumika kujenga barabara za pete kuuzunguka mji huo ili kupunguza msongamano wa magari yanayopita kwenda mikoa mingine.


“Barabara hizi husaidia kuondoa msongamano wa malori na magari makubwa hususan yanayotokea Dar-es-salaam yasiingie katikati ya jiji, yapite pembeni wakati yakienda Iringa, Singida, Arusha na kwingineko”, amesema Katambi.

Amefafanua kwa kusema kuwa shilingi bilioni 52 ni sehemu ya ulipaji fidia wananchi wanaopisha ujenzi wa uwanja wa ndege wa Msalato pia kuna ujenzi wa Chuo cha Ufundi na upanuzi wa shule ya Msingi Mpamaa. Vilevile zipo fedha awamu ya kwanza kwa ajili ya kulipa fidia kwa wananchi kupisha upanuzi wa Ikulu ya Chamwino ambapo kati ya hizo sh. bilioni 9 ilipaswa kuwa zimelipwa hadi sasa.

Amebainisha kuwa kuna ujenzi wa stendi ya mabasi ya Nzughuni, ambayo ni stendi kubwa, ya kisasa na ya kimataifa itakayoingiza mabasi 250 ambapo 100 yatakuwa yanabeba abiria na kuondoka na mengine yatabaki. Ipo sehemu ya kupumzika (VIP Lounge) ya kisasa ambayo unaweza kulinganisha na VIP ya Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere.
Fauka na hayo, stendi hiyo itakuwa na maduka makubwa (shopping mall), ofisi za kukatia tiketi za safari (booking office) na stendi itakuwa na uwezo wa kuchukua bajaji 300, pikipiki (boda boda) 150 na taxi 200 na eneo kwa ajili ya wajasiriamali wadogo 100. Kutakuwa na maeneo ya kusubiri abiria wa kawaida manne, ambapo kila eneo lina uwezo wa kuchukua abiria 150 hadi 200.

Katika stendi hiyo pia, kutakuwa na soko la kimataifa la Job Ndugai, lenye nafasi 15 za kuegesha malori, sehemu za vizimba vya wafanyabishara wanane, sita na wawili zipatazo 400, pamoja na Dodoma City Market yenye migahawa, maduka sehemu ya machinjio ya kisasa ya kuku, bucha za kisasa za nyama na maeneo ya juu kwa ajili ya ofisi. Miradi yote hiyo inakwenda sambamba na Tanzania City Strategic project ikiwemo Chinangali park, maeneo ya michezo ya mpira wa meza (table tennis), bwawa kubwa la kuogelea lenye hadhi ya Olympic lenye uwezo wa kutumiwa na watu 24 kwa wakati mmoja na uwepo wa jukwaa la muziki la kimataifa.

Miradi yote hiyo itagharimu zaidi ya shilingi bilioni 77.3 ikiwa ni pamoja na mradi wa maegesho ya magari ya watu binafsi zaidi ya 100, sehemu ya michezo ya watoto na wanyama, eneo la mpira wa miguu, migahawa nyama choma na burudani mbalimbali vyote hivyo hakuna malipo ila utalipia huduma unayopewa.













# Mahakama Yaongeza Matumizi ya Tehama Ili Kukabiliana na Corona

Mahakama ya Tanzania imeongeza kasi ya matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika shughuli zake ikiwa ni kuunga mkono hatua ya Serikali ya kuchukua tahadhari dhidi ya maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa Corona (COVID-19), ambapo sasa shughuli za mahakama zitakuwa zikifanyika kwa njia ya mtandao (Video Conference).

Jaji Mkuu wa Tanzania Profesa Ibrahim Hamis Juma amesema kwamba mahakama imeongeza maeneo ya matumizi ya TEHAMA katika kipindi hiki ambapo dunia inapita wakati mgumu wa kupambana na virusi vya Corona ambavyo vimesambaa nchi nyingi duniani.

“Mahakama imekuwa ikitumia TEHAMA katika kurahisisha shughuli zake za kutoa haki nchini licha ya kuwepo kwa ugonjwa wa Corona na baadhi ya mifumo iliyokuwa ikitumiwa ni pamoja na mfumo wa kusajili na kuratibu pamoja na kusikiliza mashauri kwa njia ya mkutano mtandao (Video Conferencing), mfumo huu ni silaha muhimu katika kuzuia mikusanyiko, misongamano na wasindikizaji wakati wa kusikilizwa kwa mashauri”, amesema Profesa Ibrahim.
Ameongeza kuwa kanuni za kufungua mashauri kwa njia ya mtandao zilianza kufanya kazi tangu tarehe 13 Aprili, 2018, na kusisitiza kuwa kanuni hizo ni muhimu kwa sasa na zitasambazwa ili wananchi na wadau watumie utaratibu huo.

Aidha, amebainisha kuwa Mahakama imeweka mitambo ya kisasa kwenye Mahakama Kuu, Masijala Kuu Dar es Salaam, Mahakama Kuu ya Mbeya, Kituo cha mafunzo Kisutu, Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto na Mahakama za Keko na Segerea, na ametoa wito kwa viongozi wote wa Mahakama katika ngazi zote kuwasaidia Watanzania kuendelea kupata huduma za utoaji haki hususan katika kipindi hiki cha msukosuko wa ugonjwa wa Corona.



# TANZANIA KINARA MAPAMBANO HALI YA HEWA NA MABADILIKO YA TABIANCHI

Tanzania imekuwa mstari wa mbele kwa nchi za kiafrika kukabiliana na changamoto za hali ya hewa na mabadiliko ya tabia nchi duniani kutokana na Serikali ya Awamu ya Tano kuimarisha Mamlaka ya Hali ya Hewa nchini.

Hayo yamesemwa na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), Dkt. Agnes Kijazi ambaye pia ni Makamu wa Tatu wa Rais Shirika la Hali ya Hewa Duniani (WMC) wakati wa kutoa taarifa yake siku ya maadhimisho hayo yanayofanyika kila mwaka tarehe 29 Machi.

"Katika eneo la vifaa vya hali ya hewa, TMA inaendelea na mkakati wake wa uboreshaji kwa kununua vifaa vya kisasa na kuondoa vifaa vinavyotumia zebaki, ambapo mkakati huo umelenga kuboresha vituo vyote vya hali ya hewa nchini ili kuendana na ukuaji wa teknolojia ya hali ya hewa duniani, ikiwa ni pamoja na kutekeleza mkataba wa Minamata (Minamata Convention) ulioanzishwa mwaka 2013 na kuanza kutekelezwa Agosti 16 2017, ambao unaozitaka nchi zote za Umoja wa Mataifa kusitisha matumizi ya zebaki kabla ya kumalizika mwaka huu wa 2020", amesema Dkt. Kijazi.

Akizungumzia maadhimisho ya siku hiyo, ametoa wito kwa wadau wote wa huduma za hali ya hewa kutoka sekta zote za kiuchumi na kijamii kuhakikisha wanaelewa na kuzitumia ipasavyo huduma hizo ili kupanga mipango ya kiuchumi na kijamii kwa ajili ya maendeleo endelevu ya Taifa. Pia, amewaomba wadau wote kuunga mkono utekelezaji wa Programu ya Kitaifa ya Huduma za Hali ya Hewa (NPCS) ili kuboresha zaidi huduma hizo hapa nchini na kupunguza athari kwa jamii na sekta ambazo zinaathiriwa moja kwa moja na mabadiliko ya hali ya hewa ikiwemo sekta ya maji.

Kauli mbiu ya mwaka huu ni "Hali ya hewa na Maji" (Climate and Water) ambayo inaenda sambamba na kauli mbiu ya Siku ya Maji Duniani kwa mwaka 2020 ambayo imejikita katika athari za mabadiliko ya hali ya hewa kwenye sekta ya maji.



# Madaktari Wamshukuru Rais Magufuli Kwa Kutekeleza Ahadi Yake

Rais wa Chama cha Madaktari Tanzania (MAT), Dkt. Elisha Osati ametoa shukrani kwa Rais John Pombe Magufuli kwa kutekeleza kwa vitendo aliyoyaahidi kwao baada ya Serikali kutangaza kutekeleza ahadi ya ajira mpya 1,000 za madaktari, iliyotolewa na Rais Magufuli Februari 20, mwaka huu na kusisitiza kwamba wako pamoja na Serikali kuiboresha sekta ya afya.

Dkt. Osati amesema kuwa chama chake kimejiandaa kikamilifu kuiunga mkono Serikali katika kutokomeza ugonjwa wa homa ya mapafu inayoletwa na virusi vya corona ambao umesambaa duniani, Tanzania ikiwemo.

" Tuko tayari kuwajibika kikamilifu kupambana na COVID-19,ambapo tangu maambukizi hayo yaingie nchini,hatua ya kwanza tuliyoanza nayo ni kutoa elimu ya ufahamu wa virusi hivyo kwa watumishi wa sekta ya afya ambapo tumeanza na watumishi wa afya katika manispaa za Temeke, Ilala na Kinondoni lengo...*inaendelea*

.... likiwa ni kuwajengea uwezo wa kumhudumia mgonjwa wa corona", amesema Dkt. Osati.

Aidha, ametoa mapendekzo yao ya kutaka madaktari watakaoajiriwa watawanywe katika maeneo yenye uhitaji mkubwa ikiwemo mipakani mwa nchi na maeneo kulikojengwa hospitali mpya.

"Tulishapendekeza hili kwa maandishi, tunaamini litazingatiwa na Wizara, maeneo ya mipakani na kwenye zile hospitali mpya kuna uhitaji mkubwa wa madaktari", amesema Dkt. Osati.

Hivi karibuni, Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mhandisi Joseph Nyamhanga alieleza kuwa Serikali imetoa nafasi za ajira kwa madaktari 610, ambazo zitatolewa kupitia maombi ya Sekretariet ya ajira.

# WIZARA YA AFYA YAPOKEA VIFAA VYA KUJIKINGA NA CORONA

Mganga Mkuu wa Serikali Profesa Muhammed Kambi, amethibitisha kupokea vifaa mbalimbali vya kupambana na kujikinga kuenea kwa virusi vya Corona kutoka kwa tajiri wa kichina Jack Ma kupitia taasisi yake ya Jack Ma Foundation.

Akivitaja vifaa hivyo, Profesa Kambi amesema kuwa vifaa vilivyopokewa vinajumuisha barakoa (mask) 100,000, vifaa kwa ajili ya vipimo na vitendanishi 20,000 na mavazi ya kujikinga wakati wa kuhudumia watu waliobainika kuwa na ugonjwa huo (protective suits) 1,000.

“Tunashukuru msaada huu, kama serikali tumekuja hapa kushuhudia sehemu ya shehena ya tani tatu ya vifaa tiba vilivyotolewa na Jack Ma Foundation ambavyo vimewasili usiku wa jana na ndege ya mizigo ya Jamhuri ya Shirikisho la Jamhuri ya Kidemokrasia ya Ethiopia (Ethiopia Airline)”, amesema Prof. Kambi.

Aidha, katika hatua nyingine Profesa Kambi alimshukuru Afisa Ubalozi wa Shirikisho la Jamhuri ya Kidemokrasia ya Ethiopia Tewodros Girma ambaye amekabidhi msaada huo kwa niaba ya Balozi wa nchi hiyo Yonas Yosef.

Taarifa aliyoitoa Waziri Mkuu wa Ethiopia Abiy Ahmed imesema kuwa vifaa tiba vitatolewa Barani Afrika kwa nchi zote 54, kwa sasa vifaa vilivyopokelewa ni pamoja na vifaa tiba milioni 1.1, barakoa (mask) milioni sita na elfu 60 ni mavazi ya kujikinga wakati wa kuhudumia watu waliobainika kuwa na ugonjwa huo (protective suits).

Aidha, vifaa hivyo vimewasili kwa ndege ya mizigo ambayo ilifika Jumapili wiki iliyopita mjini Addis Ababa na vitasambazwa katika Mataifa ya Afrika yaliyopata maambukizi ya ugonjwa wa Homa ya Mapafu ya Virusi vya Corona (COVID-19) na yanayohitaji vifaa vya kupambana na kuenea kwa ugonjwa huo. Kwa kuanzia nchi za Afrika zitakazopata msaada huo ni pamoja na Eritrea, Djibouti, Kenya, Afrika ya Kusini, Burundi, Rwanda, Togo, Zimbabwe, Nigeria na Sudani ya Kusini, hata hivyo Burundi and Sudan Kusini hawajaapata kisa chochote cha mtu aliyepata virusi vya Korona.

Tanzania imepokea msaada huo ikiwa imeshathibitisha kuwa na visa 13 vya watu wenye virusi vya Korona lakini hakuna hata mmoja aliyepoteza maisha na wote hali zao zinaendelea vizuri. Vilevile katika nchi 54 za Afrika kila moja itapokea mgao wa vifaa tiba, barakoa na nguo za kujikinga kwa idadi kama iliyopokea nchi ya Tanzania.














# Mifugo Iliyouzwa Katika Masoko Rasmi Yaingiza Sh. Bilioni 360/-

Benki Kuu ya Tanzania (BOT) imetoa ripoti ya kiuchumi inayoonesha ongezeko la idadi ya mifugo iliyouzwa kwenye masoko rasmi yanayosajili kwa kupanda na kufikia asilimia 40.6 hivyo, kuingiza kiasi cha sh. bilioni 360, mwaka 2019 ikilinganishwa na sh. bilioni 255.99 zilizoingizwa katika kipindi kama hicho mwaka 2018.

Kutokana na matokeo ya ripoti ya Kanda ya jumla ya uchumi iliyotolewa na BOT, ongezeko hilo limesajiliwa katika kanda zote za Tanzania isipokuwa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini.

Ikifafanua, ripoti hiyo imeeleza kuwa Kanda ya Kati imepanda kwa asilimia 29.9, ikifatiwa na Kanda ya Dar-es-salaam ambayo ina asilimia 26.6. Jumla ya mifugo iliyouzwa ni 739,234, kutoka Kanda ya Kati yenye thamani ya sh. bilioni 107,55, kwa robo inayoishia Septemba 2019, ikilinganishwa na mifugo 278,827, yenye thamani ya sh. bilioni 55.68 katika kipindi kama hicho mwaka 2018.

Idadi ya mifugo iliyouzwa katika kanda ya Dar-es-salaam ilikuwa 183,511, yenye thamani ya shilingi bilioni 81.5, mwaka 2019 ikilinganishwa na mifugo 104,596, yenye thamani ya shilingi bilioni 58.24, iliyouzwa kipindi kama hicho mwaka 2018.

Katika Kanda ya Ziwa mifugo iliyouzwa katika masoko rasmi yanayosajili ilikuwa 230,617, wenye thamani ya sh. bilioni 75.57, ikilinganishwa na idadi ya mifugo 257, yenye thamani ya bilioni 56.98, kwa kipindi kama hicho mwaka 2018.

Katika kipindi cha marejeo ya idadi ya mifugo iliyouzwa idadi ya ngo'mbe waliouzwa ilikuwa 602,471, yenye thamani ya sh. bilioni 328.74, ikilinganishwa na ng'ombe waliouzwa wenye thamani 234.84, kwa robo iliyoishia Septemba 2018.

Idadi ya mbuzi waliouzwa walikuwa 356,586, wenye thamani ya bilioni 24.21, mwaka 2019, ikilinganishwa na mbuzi 280,546, wenye thamani ya bilioni 15.66 na idadi ya kondoo waliouzwa kipindi hicho ni 122.038, wenye thamani ya bilioni 7.05, ikilinganishwa na 99.453 kondoo wenye thamani ya bilioni 5.49 mwaka 2018.



# Kuanzishwa Kwa Shamba la Mianzi Ruvu Kaskazini ni Fursa ya Biashara Tanzania

Benki Kuu ya Tanzania (BOT) imetoa ripoti ya kiuchumi inayoonesha ongezeko la idadi ya mifugo iliyouzwa kwenye masoko rasmi yanayosajili kwa kupanda na kufikia asilimia 40.6 hivyo, kuingiza kiasi cha sh. bilioni 360, mwaka 2019 ikilinganishwa na sh. bilioni 255.99 zilizoingizwa katika kipindi kama hicho mwaka 2018.

Kutokana na matokeo ya ripoti ya Kanda ya jumla ya uchumi iliyotolewa na BOT, ongezeko hilo limesajiliwa katika kanda zote za Tanzania isipokuwa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini.

Ikifafanua, ripoti hiyo imeeleza kuwa Kanda ya Kati imepanda kwa asilimia 29.9, ikifatiwa na Kanda ya Dar-es-salaam ambayo ina asilimia 26.6. Jumla ya mifugo iliyouzwa ni 739,234, kutoka Kanda ya Kati yenye thamani ya sh. bilioni 107,55, kwa robo inayoishia Septemba 2019, ikilinganishwa na mifugo 278,827, yenye thamani ya sh. bilioni 55.68 katika kipindi kama hicho mwaka 2018.

Idadi ya mifugo iliyouzwa katika kanda ya Dar-es-salaam ilikuwa 183,511, yenye thamani ya shilingi bilioni 81.5, mwaka 2019 ikilinganishwa na mifugo 104,596, yenye thamani ya shilingi bilioni 58.24, iliyouzwa kipindi kama hicho mwaka 2018.

Katika Kanda ya Ziwa mifugo iliyouzwa katika masoko rasmi yanayosajili ilikuwa 230,617, wenye thamani ya sh. bilioni 75.57, ikilinganishwa na idadi ya mifugo 257, yenye thamani ya bilioni 56.98, kwa kipindi kama hicho mwaka 2018.

Katika kipindi cha marejeo ya idadi ya mifugo iliyouzwa idadi ya ngo'mbe waliouzwa ilikuwa 602,471, yenye thamani ya sh. bilioni 328.74, ikilinganishwa na ng'ombe waliouzwa wenye thamani 234.84, kwa robo iliyoishia Septemba 2018.

Idadi ya mbuzi waliouzwa walikuwa 356,586, wenye thamani ya bilioni 24.21, mwaka 2019, ikilinganishwa na mbuzi 280,546, wenye thamani ya bilioni 15.66 na idadi ya kondoo waliouzwa kipindi hicho ni 122.038, wenye thamani ya bilioni 7.05, ikilinganishwa na 99.453 kondoo wenye thamani ya bilioni 5.49 mwaka 2018.